II. الْحَرْفِيّ **Al-Harfiyy: (ya neno)**

الْمَد اللّازِمْ الْحَرْفِيّ **Al-Madd Al-Laazim Al-Harfiyy** ni madd inayopatikana katika herufi zilizokuja kwenye mwanzo wa Suwrah 29 za Qur-aan zinazoitwa: الْحُرُوف الْمُقَطَّعة Al-Huruwf Al-Muqatw-twa'ah (Herufi zilizokatika) kwa maana zinatamkwa kama herufi za hijaaiyyah. Jumla ya herufi hizo ni 14 ambazo zimeundwa katika ibara kadhaa mojawapo ni:

طرق سمعك النصيحه

Baadhi ya hizi Al-Huruwf Al-Muqatw-twa'ah zimekariri zaidi ya mara moja na kuzifanya jumla kuwa ni ishirini na tisa:

الٓمٓ الٓمٓصٓ الٓر الٓمٓر كٓهيعٓصٓ طه طسٓمٓ طسٓ

يسٓ صٓ حمٓ حمٓ ﴿١﴾ عٓسٓقٓ ﴿٢﴾ قٓ نٓ

Herufi hizi zimegawika sehemu nne:

- Isiyo na madd nayo ni ا (الف) Alif -haivutwi kabisa.
- Madd harakah mbili katika herufi za حي طهر [1]
- Madd haraka mbili au nne au sita katika herufi ya ع (عين) kwa kuwa inatekelezwa kwa مَدُّ اللِّين (maddul-liyn)
- Madd harakah sita katika herufi za سنقص لكم

(سين – نون – قاف – صاد – لام – كاف – ميم)

Imegawanyika katika sehemu mbili:

[1] Rejea mlango wa Maddutw-twabiy'iy - Alifaatu-Hayyin-Twahur

**الْمَدُّ اللاَّزِمِ الْحَرْفِيّ الْمُثَقَّل -Al-Madd Al-Laazim Al-Harfiyy Al-Muthaqqal** na **المد اللّازِمِ الْحَرْفِيّ الْمُخَفَّف - Al-Madd Al-Laazim Al-Harfiyy Al-Mukhaffaf**